



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA AFYA

BARAZA LA FAMASI



TAARIFA KWA UMMA

**KUONGEZWA KWA MUDA WA KUHUISHA VIBALI VYA FAMASI KWA MFUMO WA
KILEKTRONIKI KWA MWAKA 2024/25**

DODOMA: 14 Julai, 2024

Kifungu Na. 36 cha Sheria ya Famasi, Sura 311 kinaelekeza kuwa jengo la biashara ya Famasi lililosajiliwa na Baraza la Famasi kuhuisha leseni ya biashara kila ifikapo tarehe 30 Juni ya kila mwaka.

Tarehe 06 Juni, 2024 Ofisi ya Msajili ilifungua dirisha la uhuishaji wa leseni za biashara za maduka ya Dawa kwa Mwaka 2024/25 na kumalizika ifikapo tarehe 15 Julai, 2024.

Kutokana na changamoto iliyojitokeza katika mfumo (***Pharmacy Council Information Management System – PCMIS***) kushindwa kutoa ankara za malipo (*Control number*) iliyosababishwa na kukatika kwa mkongo wa mtandao wa serikali katika maeneo ya Ofisi za Baraza za Kanda ya Mashariki (Dar es Salaam), ofisi inapenda kuwatangazia wamiliki na wafamasia wasimamizi wa Maduka ya Dawa kuwa, imeongeza muda wa uhuishaji wa leseni za biashara za maduka ya Dawa hadi ifikapo tarehe **30 Julai, 2024**.

Tunaomba radhi kwa usumbufu wowote uliojitokeza wakati wote changamoto hii ilipokuwa inashughulikiwa. Hivyo, tunawasihi wafamasia wasimamizi na wamiliki wa maduka ya dawa kuhakikisha wanakamilisha uhuishaji kabla ya tarehe iliyotajwa hapo juu.

Imetolewa na:

Msajili, Baraza la Famasi

S.L.P. 1277,

Dodoma

Namba ya mawasiliano bila malipo 0800110015